

## Maswali

1. Mbona Mungu aliwakasirikia Waisraeli?
2. Waisraeli walinukunika kwa nini?
3. Kwa kuwaadhibu Mungu alituma nini?.
4. Nini ilifanyika wakati Waisraeli waliumwa na nyoka?
5. Waisraeli walitaka Musa afanye nini?
6. Mungu aliondoa nyoka?
7. Mungu alisema atafanye nini tena?
8. Mungu alimwambia Musa afanye nini?
9. Waisraeli waliponywa namna gani?
10. Ni somo gani Mungu anatufundisha juu ya Yesu?

## Majibu

1. Mungu alikasirika kwa sababu Waisraeli walinun'gunika tena.
2. Huo mwendo ulikuwa mgumu. Walitaka maji mengi na walichoka na mana.
3. Mungu alituma nyoka wa moto kuwaadhibu Waisraeli.
4. Waliugua kwa uchungu na kukufa.
5. Waisraeli walitaka Musa awaombe kwa Mungu.
6. Ndiyo Mungu aliondoa hizo nyoka za moto
7. Mungu alisema atawaponya watu walioumwa.
8. Mungu alimwambia Musa atengeneze nyoka ya shaba kwa mti
9. Waisraeli waliponywa kwa kuamini Mungu na kwa kuangalia nyoka ya shaba.
10. Yesu aliinuliwa msalabani ili tukiamini na kutii Mungu tutaokoka.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



# 6 Nyoka ya shaba

## Marejeo

Hesabu 21:4-9; Yohana 3:14-16

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu anaokoa watu wake wenye imani.

## Maneno maalum

1. Jangwani + choka + nun'gunika
2. Mungu anakasirika + linda + peana + hakuna shukrani
3. Nyoka ya moto + uma watu + ugua
4. Tumefanya dhambi + samehe + nyoka ya shaba
5. Mti + enda + angalia + pona
6. Amini + jaribu + pona
7. Hakuna imani + kifo + uponyaji kutoka kwa Mungu
8. Yesu + msalaba + amini + ishi

**6.1** Waisraeli walisafiri jangwani. Kutoka nyikani walikwea kwa miamba ilio karibu na mtelemko wa bahari ya Shamu. Baada ya mda Waisraeli walichoka. Walinun'gunikia Musa wakisema huo mwendo ni mgumu kwao. Tena walinun'gunika kwamba hawakuwa na maji ya kutosha. Walisema kwamba wamechoka na mana waliyotumiwa na Mungu wale kila siku. Walisema walikula vitu vingi sana huko Misri. Walitamani kurudi huko Misri.

**6.2** Mungu aliwakasirikia wana Waisraeli. Alikuwa amewaokoa kutoka Misri. Aliwalinda kwa safari yote ya jangwani. Aliwapa maji ya kunywa. Kila asubuhi aliwaletea mana wale. Lakini Waisraeli hawakushukuru Mungu. Hawakuamini Mungu wakati jambo lolote lilienda mrama, walinungunika.


**6.3** Mungu aliwatumia kwa kambi nyoka wa moto wabaya. Hao nyoka wa moto walipotokea. Waisraeli walikimbia wakilia wakielekea kwa mahema. Lakini nyoka walijinyonga nyoga mpaka ndani ya mahema. Nyoka wakawauma na kwa sababu walikuwa wa sumu, watu wengi walikufa. Wengine walibaki hemani wagonjwa kwa kuunwa na nyoka. Waliunia sana. Waliogopa wote kwa sababu hawakujua wakati nyoka wangekuja na kuwauma. Huko kambini watu waliugua na kulia kwa sauti ya hofu.

**6.4** Wana Waisraeli waliogopa. Hao nyoka wa moto walikuwa kila pahali kambini. Waliendelea kuwauma. Waisraeli walimwendea Musa. Wakasema, "Tumetenda dhambi, tulikosa kunun'guka. Tafadhali tuombe kwa Mungu na umwambie atusamehe. Tafadhali ambia Mungu atuondolee hawa nyoka wa moto." Musa aliomba Mungu. Mungu akasikia maombi ya Musa na kuondoa wale nyoka wa moto. Ingawaje kulikuwa na watu wengi waliokuwa wagonjwa kwa ajili ya kuumwa na nyoka.



Mungu alikuwa mzuri na akasema kwamba atawaponya. Akaambia Musa atengeneze mfano wa nyoka kutoka kwa shaba na aiweke kwa mti. Mungu akawambia yeyote atakaye umwa na nyoka na aangalie nyoka ya shaba mtini atapona.

**6.5** Musa alitengeneza huyo nyoka wa shaba haraka sana. Akaiweka kwa mti. Musa akaambia Waisraeli kwamba Mungu ataponya waliokuwa wagonjwa kutokana na kuumwa na nyoka. Musa aliwaambia yeyote atakaye umwa ni lazima angalie nyoka ya shaba. Wakiangalia nyoka ya shaba wataponywa. Musa aliweka hiyo nyoka ya shaba juu sana kwa mti ili kila mtu aione.



**6.6** Nyoka wa moto walikuwa wamewauma wana wa Israeli wengi. Waliugua sana Walikuwa na uchungu mwingi sana, lakini waliamini kwamba Mungu atawaponya. Walijaribu kutoka vitandani na kuenda nje ya hema. Waliangalia nyoka ya shaba juu ya mti. Walipoona nyoka ya shaba walipona.

**6.7** Waisraeli wengine hawakuamini kwamba watakapoangalia nyoka ya shaba wangepona. Hawakujaribu kutoka hemani na kuenda nje. Hao walikufa kwa kuumwa na nyoka. Nyoka ya shaba haikuwa ya mwujiza, nyoka ya shaba ilikuwa kibande cha chuma. Haingeponya mtu yeyote. Ni Mungu ndiye aliponya watu. Ilibidi watu waamini Mungu na kumtii ili waponywe.

**6.8** Mungu anatufundisha somo katika hadithi hii ya nyoka ya shaba. Anatufundisha somo juu ya Yesu. Nyoka ya shaba iliinuliwa juu ya mti kila mtu aliyeamini akaiangalia hakukufa. Walipona na wakaishi. Yesu aliinuliwa juu msalabani. Kila mtu amwaminie Yesu na kumtii Mungu hatakufa milele, atakuwa na uzima wa milele.